

Elimu, Sayansi na Teknolojia

58. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imewezesha ujenzi wa madarasa 15,000 katika shule za sekondari na vituo shikizi na mabweni 50 kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum. Ujenzi wa miundombinu hii umewezesha wanafunzi wote 907,803 waliofaulu mtihani wa darasa la saba mwaka 2021 kupata nafasi ya kuanza kidato cha kwanza Januari 2022 bila kusubiri chaguo la pili. Kadhalika, Serikali imekamilisha maboma 560 ya vyumba vya madarasa katika shule za sekondari kutokana na tozo za miamala ya simu ambapo shilingi bilioni 7.0 zilitolewa; Aidha, Serikali imetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 569 kwa wanafunzi 177,777 wa elimu ya juu.

assengaonline.com

59. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2022/23 Serikali itaenda kutekeleza mradi wa “*Higher Education for Economic Transformation*” (HEET) wenye thamani ya dola za Marekani milioni 425. Mradi huu utahusisha ujenzi wa miundombinu katika vyuo vikuu mama na katika mikoa kadhaa ambayo haina vyuo vikuu ikiwemo Lindi, Kagera, Rukwa, Katavi, Manyara na kukamilisha ujenzi wa *Institute of Marine Science Zanzibar* na kujenga chuo kipya cha TEHAMA Dodoma.

60. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kugharamia programu ya elimumsingi bila ada ambapo hadi Aprili 2022,

jumla ya shilingi bilioni 244.5 zilitolewa. **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan** Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa CCM ameguswa sana na watoto kukatisha masomo kwa ajili ya sababu mbalimbali. Miongoni mwa sababu zinazosababisha kukatisha masomo ni umaskini wa kipato kwenye familia zetu, mimba za utotoni, mwamko duni wa elimu kwa baadhi ya jamii na utoro na wale wasioendelea kufuatana kwa mujibu wa sheria (Ufaulu). **Ili kukabiliana na utoro (drop out) wa wanafunzi wanaotoka familia maskini**, bado tuna watoto wanaoshindwa kumudu mahitaji ya lazima licha ya kuwepo kwa programu ya elimu bila malipo na hivyo wanasaidiwa na wabunge, madiwani na wengine kuchangiwa na wasamaria wema. **Napendekeza kuanzisha dirisha maalum (Special Fund) kupitia TASAF itakayosaidia watoto wanaotokea familia maskini.** Kwa msingi huo napendekeza kuanza na bilion 8 kwa ajili ya watoto masikini watakaopatikana kwenye database ya TASAF na taarifa za wabunge na madiwani.

61. **Mheshimiwa Spika**, ili kukabiliana na mimba za utotoni, Serikali itaendelea kujenga mabweni kwenye maeneo hatari kwa watoto wa kike. Aidha, ili kutoa fursa kwa watoto wasioendelea na vidato na vyuo, Serikali itaendelea kuimarisha elimu ya ufundi hususan katika vyuo vya kati kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kujajiri ama kuajiriwa. Mpaka sasa Wilaya 77 zina vyuo vya Ufundi VETA kati ya Wilaya 138 nchini kote. Tuna mikoa 25 ina Vyuo vya Ufundi kati ya mikoa

26. Bado mkoa wa Songwe hauna kabisa Chuo cha VETA na wabunge wa mkoa wa Songwe wamekuwa wakishinda Ofisini wakifuatilia ahadi waliopewa na Mheshimiwa Rais. Bado kuna wilaya 36 ambazo hazina vyuo wala vyuo vya Mkoa. Napendekeza kutoa bilioni 100 kwa ajili ya ujezi wa vyuo vya ufundi kwa Mkoa wa Songwe na wilaya 36 ambazo hazina vyuo ili kufanya wilaya zote 138 kuwa na chuo cha Ufundi (VETA). **Waheshimiwa wabunge, Huyo ndio SAMIA.**

62. **Mheshimiwa Spika**, kwa sasa wanafunzi wa kidato cha tano ni takriban 90,825 na kidato cha sita ni 56,880. Mahitaji ya fedha ni shilingi **10,339,350,000**. Ili kuwapunguzia gharama watoto hao kama **Mheshimiwa Rais** alivyoielekeza Wizara, **napendekeza kufuta ADA kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita. Kwa hatua hiyo, Elimu bila Ada ni kuanzia shule za msingi mpaka kidato cha sita.** Serikali itajipanga kuangalia namna ya kusaidia vyuo vya kati **kadiri** hali ya uchumi itakavyotengemaa. Nani kama SAMIA? Nani kama Mama? Nani kama CCM? CCM ni Na. 1.